Jarida la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania

# TARI HABARI

UTAFIFI KWA MAENDELEO YA KILIMO

ISBN: 978-9912-42-694-8 | Toleo No. 02 Oktoba - Desemba 2025 | www.tari.go.tz



# TARI YAWAONGOZA WADAU WA KILIMO KUADHIMISHA SIKU YA UDONGO DUNIANI MWAKA 2025



Mhe. Chongolo ataka watafiti wagunduzi wa mbegu za kilimo wanufaike na utafiti wao



Bila utafiti imara hakuna tija kwenye kilimo: Dkt. Bwana



TARI yatoa Mbegu bora za miwa kwa wakulima kilombero

TARI Transforming Agriculture

## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**

DKT. THOMAS BWANA
Mkurugenzi Mkuu TARI

**KATIBU**

DKT. SOPHIA KASHENGE
Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia, Biashara na Mahusiano

**WAJUMBE**

EVELYNE MPASHA
Kaimu Meneja Menejimenti ya Maarifa na Mawasiliano

DKT. RAJAB KANGILE
Kaimu Meneja wa uhaulishaji wa teknolojia, uendeshaji wa biashara na ushirikiano

DKT. ABDULLAH MKIGA
Kaimu Meneja wa Kituo, TARI Kifyulilo

DKT. ANDEKILILE MWAMAHONJE
Mtafiti Mwandamizi

DEODATUS KIRIBA
Mtafiti Mwandamizi

**WAANDISHI**

GERALD USIRI
Afisa Mahusiano kwa Umma

MUGINI A. SINGIRA
Afisa Mahusiano kwa Umma

HOSEA R. BILATANGUYE
Afisa Mahusiano kwa Umma

TariTanzania | Tanzaniatari | official_taritanzania | TariTV

# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

**NDUGU** msomaji na wadau wa sekta ya kilimo,

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru nyote kwa ushirikiano, dhamira na mchango mkubwa mnaoendelea kutoa katika kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kutimiza majukumu yake ya msingi ya kuzalisha, kuendeleza na kusambaza teknolojia bora za kilimo kwa wakulima na wadau wengine nchini.

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka, TARI imefanikiwa kutekeleza shughuli muhimu kadhaa ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa uzalishaji na tija kwenye sekta ya kilimo. Baadhi ya mafanikio muhimu ni pamoja na:

Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia:

TARI imeendelea kufanya tafiti shirikishi katika mazao ya kipaumbele, kuendeleza mbegu bora zenye ustahimilivu wa visumbufu na mabadiliko tabianchi, pamoja na teknolojia za kuongeza thamani ya mazao.

Hii imewezesha kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, taarifa za kiteknolojia kwa wakulima na kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

Kusambaza Teknolojia kwa wadau kupitia maonesho, mafunzo ya wakulima, kliniki za mimea na ziara za kimafunzo:

Taasisi imefikisha teknolojia na maarifa mapya kwa maelfu ya wakulima katika maeneo mbalimbali nchini. Hatua hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji na kupunguza hasara kwa wakulima.

Katika kipindi cha Robo ya kwanza TARI imefanikiwa kutekeleza Miradi mbalimbali ikiwemo katika kuendelea na Utafiti wa Aina 42 za mbegu tarajali (Promising lines) za mahindi, maharage, mpunga, mtama, muhogo, zabibu, ndizi na mchicha zimewasilishwa katika Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) kwa ajili ya majaribio ya utambuzi wa mbegu mpya (DUS) na majaribio ya umahiri wa mbegu (NPT). Nasaba 27,505 za mazao mbalimbali zimeendelea kutuzwa kwa ajili ya shughuli ya Utafiti na mbegu. Kuendelea na majaribio ya Utafiti na ugunduzi wa Teknolojia. Utafiti huo umejikita katika ugunduzi wa teknolojia bora za mbegu, magonjwa na afya ya Udongo.

Pia katika Uzalishaji wa mbegu na Miche Tani 483,436 za mbegu za awali za mazao mbalimbali ya kimkakati na miche 756,148 ya mazao mbalimbali imezalishwa.



*DKT. THOMAS BWANA*
*MKURUGENZI MKUU - TARI*

Aidha, Uhaulishaji wa teknolojia, Teknolojia ya Kitalu mkeka imehaulishwa katika maonesho ya Sabasaba na Nanenane kupitia mashamba darasa (demonstration plots) na siku ya wakulima (farmers field day), mafunzo kwa wakulima na maafisa ugani teknolojia mbalimbali zimehaulishwa.

Ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa:

TARI imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuboresha miundombinu ya utafiti, kuongeza ubunifu, na kuhakikisha kuwa tafiti zetu zinaendana na viwango vya kimataifa.

Utawala na Uboreshaji wa Miundombinu: Taasisi imefanikiwa kuimarisha mifumo ya usimamizi, matumizi ya TEHAMA, na kuboresha baadhi ya miundombinu ya vituo vya utafiti ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu.

Tunatambua bado kuna changamoto katika maeneo kama upatikanaji wa rasilimali, mabadiliko ya tabia ya nchi, na kasi ya kusambaza teknolojia kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, tumejipanga kuendelea kuyashughulikia kwa kuongeza ubunifu, ushirikiano, na matumizi ya utafiti unaoendeshwa na mahitaji ya wadau.

Nawashukuru wafanyakazi wote wa TARI, washirika wa maendeleo, taasisi za serikali na zisizo za serikali, pamoja na wakulima wetu kwa ushirikiano unaoendelea. Tujenge misingi imara ya kilimo chenye tija, kinachochangia uchumi wa taifa na ustawi wa wananchi.

Nakukaribisha mdau wetu katika Jarida letu la "TARI HABARI" toleo la pili ili uweze kupata habari za kitafiti na teknolojia za TARI.

***TARI - Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo.***

# TARI YAWAONGOZA WADAU WA KILIMO KUADHIMISHA SIKU YA UDONGO DUNIANI MWAKA 2025

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imewaunganisha wadau mbalimbali wa sekta ya Kilimo nchini kuadhimisha siku ya udongo duniani kwa mwaka 2025 ambayo ilibebwa na kauli mbiu isemayo " Udongo wenye afya kwa Miji Maridhawa".

Maadhimisho hayo ambayo yalifanyika kwa ngazi ya kitaifa kwa siku tatu mfululizo, kuanzia Disemba 3 hadi 5, Jijini Dodoma yalijumuisha matukio mbalimbali, ikiwemo mikutano na mafunzo maalumu juu ya afya ya udongo kwa wakulima na wanafunzi wa shule za Sekondari, upimaji wa udongo na njia bora za utunzaji udongo pamoja na zoezi la upandaji miti katika Shule ya Sekondari Dodoma.

Awali akifungua maadhimisho hayo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Steven Nindi, aliipongeza TARI kwa kuratibu maadhimisho hayo mwaka 2025




na kuagiza Taasisi na Wizara zote zinazoguswa na sekta ya udongo nchini kushirikiana kwa karibu katika kuandaa maadhimisho yajayo Ili kukuza ustawi wa sekta hiyo muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini

*"Itapendeza sana kama katika maadhimisho yajayo wadau wengi zaidi watahusishwa katika maandalizi ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Tafiti za Misitu Tanzania (TAFORI), Taasisi za Elimu ya Juu, NGO pamoja na wadau wengine wanaojihusisha na masuala ya udongo toka ndani na nje ya nchi ili kubadilishana uzoefu" alisema Dkt. Nindi.*

Katika hatua nyingine, Dkt. Nindi aliwapongeza walimu na wanafunzi wa shule za Sekondari walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Udongo Duniani kwa mwaka 2025, na kuongeza kuwa hatua hiyo inatoa taswira chanya kwa mendeleo ya sekta hiyo kwa vizazi vijavyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alisema TARI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imepata fursa na heshima ya kuwa mwenyeji wa kuandaa maadhimisho hayo kwa mwaka 2025 kwa kushirikiana na wataalamu na wadau mbalimbali wanaojihusisha na masuala ya udongo.

Dkt. Bwana ameishukuru Serikali kwa kuipatia TARI fedha kwa ajili ya kuzifanyia maboresho maabara za udongo kwenye vituo vya TARI na kuongeza kuwa pindi ukarabati huo utakapokamilika TARI itakuwa na uwezo mkubwa wa kupima sampuli nyingi zaidi za udongo kwa kutumia vifaa vya kisasa.

*"Kwa sasa, TARI inayo maabara ya kisasa ya kupimia afya ya udongo iliyopo katika kituo chetu cha TARI Mlingano, Mkoani Tanga, ambayo hivi karibuni inatarajia kupata ithibati kutoka Taasisi ya Huduma za Ithibati za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, yaani Southern Africa Development Community Accreditation Services," alisema Dkt. Bwana.*

Kuhusu utekelezaji wa afua mbalimbali za kuboresha sekta ya udongo nchini Tanzania, Dkt. Bwana alieleza kuwa TARI inafanya kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo, pamoja na Taasisi na wadau wengine muhimu kutoka sekta za Umma, na binafsi nchini ili kuwasaidia wakulima kuelewa aina za mazao yanayopaswa kuzalishwa kwenye maeneo yao,



aina za mbegu na mbolea, kiwango cha maji kinachostahili, pamoja na pembejeo zinazofaa kutumika.

**SALAM**

Akitoa salamu zake, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Profesa Peter Msoffe alisema ofisi yake inahusika moja kwa moja na swala zima la afya ya udongo na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu na TARI, Wizara ya Kilimo, pamoja na Taasisi na Wizara zote zinazoguswa na swala la afya ya udongo katika kupanga na kutekeleza afua mbalimbali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Rasilimali za Malisho ya Mifugo Kutoka Wizara ya Mifugo, Dkt. Asimwe Rwiguza, katika salamu zake kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi alisema ustawi wa sekta ya Mifugo kwa kiasi kikubwa unategemea uwepo wa udongo wenye afya.

"Bila kuwepo udongo wenye afya hakuna namna yoyote ambayo chakula cha mifugo (Malisho) kinaweza kuzalishwa,"

Kwa msingi huu, alisema Wizara ya Mifugo itaendelea na jitihada mbalimbali za kuweka mikakati ya kutekeleza afua muhimu za kuifadhi afya ya udongo kwa kushirikiana na TARI, pamoja na wadau wengine husika.

## MAAGIZO YA SERIKALI KWA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI) JUU YA UBORESHAJI, UENDELEZAJI NA ULINZI WA AFYA YA UDONGO NCHINI

SERIKALI, kupitia Wizara ya Kilimo imeiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kujikita katika utekelezaji wa mikakati kadhaa Ili kuchochea kasi ya uhifadhi wa afya ya udongo nchini Tanzania.

Maagizo hayo yanayolenga kuboresha tija na uzalishaji katika sekta za Kilimo na Mifugo, yametolewa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo, Dkt. Steven Nindi wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Udongo duniani yaliyofanyika kwa ngazi ya Kitaifa Jijini Dodoma tarehe 3 Disemba, 2025.

Miongoni mwa maagizo yaliyotolewa na kuelekezwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomasi Bwana ni pamoja na :-

- ***TARI kubuni na kuendeleza teknolojia za kilimo sahihi, za kisasa na rafiki kwa mazingira na afya ya udongo;***
- ***TARI kuharakisha mchakato wa upimaji na utoaji wa matokeo ya tathmini ya afya ya udongo nchi nzima, ambapo mpaka sasa sampuli zaidi ya elfu 52 zimeshakusanywa na zipo kwenye maabara mbalimbali za udongo ikiwemo TARI Mlingano;***
- ***TARI kushirikiana na wazalishaji, waagizaji wa pembejeo za kilimo ili kuhakikisha pembejeo zinazopelekwa kwa wakulima haziathiri ustawi wa afya ya udongo;***
- ***TARI kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) pamoja na watunga sera katika mchakato wa kutengeneza ramani mpya ya taifa ya ardhi ya kilimo na mifugo;***
- ***TARI kushirikiana na sekta binafsi katika kuboresha utekelezaji na ufanisi wa afua mbalimbali za ustawi wa afya ya udongo nchini Tanzania;***
- ***TARI kuhakikisha wakulima wanapata taarifa sahihi na kwa wakati juu ya aina za mazao, mbegu, viatilifu na viwango vya maji vinavyotakiwa kulingana na aina na afya ya udongo katika maeneo yao ya uzalishaji.***

# MHE. CHONGOLO ATAKA WATAFITI WAGUNDUZI WA MBEGU ZA KILIMO WANUFAIKE NA UTAFITI WAO

**WAZIRI** wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt. Thomas Bwana kuandaa utaratibu utakaowezesha watafiti wagunduzi wa mbegu za kilimo wananufaika na tafiti walizogundua ambazo zina tija kwa wakulima na Sekta ya kilimo kwa ujumla.



Mhe. Chongolo ametoa mfano wa Mtafiti aliyegundua mbegu ya pareto ambaye hanufaiki na matokeo ya utafiti wake, na kutaka utaratibu uandaliwe ili mtafiti huyo pamoja na watafiti wengine waweze kupata motisha na kufaidi matunda ya kazi waliyofanya.

"Watafiti wengi wagunduzi wamekuwa wakitumia muda mwingi kufanya tafiti ambazo matokeo yake yana tija kwa muda mrefu, wengine wanastaafu na wengine wanafariki bila kunufaika na kazi walizofanya, hili lichukuliwe kwa uzito na mimi nitalisimamia kwa ukaribu zaidi" alisema Mhe. Chongolo.

Mhe. Chongolo ametoa agizo hilo alipokutana na Menejimenti za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Menejimenti ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) pamoja na Menejimenti ya Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) Novemba 24, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Kilimo Jijini Dodoma wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa Taasisi hizo pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali ya kutaka Sheria za Taasisi hizo kusomana ili kuleta tija katika utatuzi wa changamoto za wakulima.




Awali akiwasilisha utekelezaji wa majukumu ya TARI, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alieleza kuwa kwa sasa TARI ina upungufu wa wataalam wabobezi kwa sababu ya kustaafu, hatua ambayo ilipelekea Waziri wa Kilimo kuagiza wataalamu hao wabobezi, waongezewe umri wa kustaafu ili watumie utaalamu wao kuwajengea uwezo watafiti chipukizi.

Katika hatua nyingine, Mhe. Chongolo ameagiza Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Kilimo kukamilisha miradi inayoendelea katika Tasisi zao kwa sasa na kuhakikisha inaleta tija kabla ya kuanzisha miradi mipya.

Kikao hicho cha uwasilishaji majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo kilihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde, Katibu Mkuu Mhe. Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Ushirika na Umwagiliaji Mhe. Athuman Kilundumya pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Kilimo.





# TARI SELIAN NA BIVAC WAWAWEZESHA WAKULIMA NA WAJASIRIAMALI KUPITIA MAFUNZO YA KUONGEZA THAMANI YA ZAO LA NGANO

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania kupitia Kituo cha TARI Selian kwa kushirikiana na BIVAC imeendesha mafunzo maalumu kwa wakulima na wajasiriamali 35 kuhusu kuongeza thamani ya zao la ngano ikiwa ni hatua ya kukuza tija na kipato kwa vijana na wadau wa kilimo nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Ngano kutoka Kituo cha TARI Selian, Bw. Ismail Ngolinda, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wakulima na wajasiriamali kupata mbinu bora za kijasiriamali katika kuongeza thamani ya mazao, hasa zao la ngano. Aliongeza kuwa mafunzo hayo yalihusisha pia mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora za zao hilo.

Akiogelea kuhusu elimu iliyotolewa wakati wa mafunzo hayo, Bi. Neema Lyimo ambaye ni mtafiti kutoka Kituo cha TARI Selian alieleza kuwa washiriki walijifunza kwa vitendo utayarishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na zao la ngano kama vile sambusa, maandazi, chapati, pilau Pamoja na makande.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa BIVAC, Bi. Beatrice Msafiri, alieleza kuwa mafunzo hayo kwa wakulima na




wajasiriamali yamelenga si tu kuongeza thamani ya mazao bali pia kuongeza kipato cha wakulima na wajasiriamali ili kuleta tija zaidi katika sekta ya kilimo nchini ili kuendana na dhana ya Kilimo Biashara.

Katika kuhakikisha bidhaa zinawekwa katika vifungashio vilivyo bora, Mtafiti Bi. Upendo Titi kutoka TARI Selian amewashauri wakulima na wajasiriamali kuwa wabunifu na kuzingatia ufungashaji bora wa bidhaa zao pamoja na utunzaji wa kumbukumbu za mauzo ili kuongeza thamani ya bidhaa zao.

Katika hatua nyingine, Afisa kilimo wa zao la ngano kutoka Wilaya ya Siha Bi. Joan Ugawa kwa niaba ya washiriki wote aliwashukuru TARI Pamoja na BIVAC kwa mafunzo na ujuzi waliopatiwa na kuahidi kutumia elimu waliyoipata katika kuboresha bidhaa na kuongeza kipato chao.

Washiriki wa mafunzo hayo walitoka katika Wilaya za Siha- Kilimanjaro, Monduli – Arusha, Arumeru – Arusha, Karatu – Arusha na Hanang – Manyara.




# OFISI YA WAZIRI MKUU, TARI ZASHIRIKIANA KUTOA MAFUNZO YA KILIMO

**OFISI** ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu (KVAU) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) wameanza kutoa mafunzo kwa wakulima na waongeza thamani katika mazao mbalimbali kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya kilimo.

Akizungumza katika ufunguzi rasmi wa mafunzo hayo uliofanyika Oktoba 21, 2025 Jijini Dodoma, Naibu katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu Bi. Zuhura Yunus amesema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kutoa huduma bora zaidi katika sekta ya kilimo.

Ametaja Mikoa itakayofanyika mafunzo hayo na mazao husika kuwa ni Dodoma zao la Zabibu, Singida zao la Alizeti, Iringa zao la mchicha lishe na nyanya, Mkoa wa Mbeya matumizi ya mitambo midogo ya kilimo, Maharage na parachichi ambapo jumla ya Wakulima elfu moja wanatarajiwa kunufaika na mafunzo hayo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana ameshukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuitambua TARI na kuipatia jukumu la kuendesha mafunzo hayo suala ambalo ameahidi kulitekeleza kwa ufasaha kupitia wataalamu wake katika maeneo husika.

Wakitoa neno la shukrani kwa nyakati tofauti, wanufaika wa mafunzo hayo wamepongeza Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na TARI kuendesha mafunzo hayo ambayo wanasema yatawasaidia kuongeza tija katika kilimo kwa kukifanya kibiashara.









# TARI YATOA MBEGU BORA ZA MIWA KWA WAKULIMA KILOMBERO

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia kituo chake cha TARI Kibaha imetoa zaidi ya tani 300 za mbegu bora za miwa aina ya R 570 kwa wakulima 60 wa Walaya ya kilombero mkoani Morogoro,ikiwa ni juhudi za kuongeza uzalishaji na kuinua kipato cha wakulima kupitia kilimo chenye tija.

Akizungumza wakati wa utoaji wa Mbegu hizo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Meneja wa Utafiti wa Rasilimali asili na Uhandisi Kilimo Dkt, Hildelitha Msita amesema mbegu za R 570 zina ubora wa hali ya juu na zimekuwa zikionesha matokeo mazuri katika uzalishaji.



Dkt. Msita ameongeza kuwa kwa sasa wameanzisha shamba la uzalishaji wa mbegu za miwa Kijiji cha Ichonde kisawasawa,wilaya ya kilombero lenye ukubwa wa Ekari nne, ambalo linatarajiwa kuongeza upatikanaji endelevu wa mbegu bora kwa wakulima.

Aidha, Dkt. Msita, alitoa wito kwa wakulima kuhakikisha wanatumia mbegu za R 570 ili kuongeza tija, kuongeza mavuno na hatimaye kuboresha kipato cha mtu moja kwa moja.





Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Mhe, Wakili, Dunstan Dominik Kyobya ameishukuru TARI kwa kugawa mbegu hizo huku akiwashauri Wananchi wa Kilombero kuchangamkia fursa ya kutumia mbegu bora zinazozalishwa na TARI kwa ajili ya kupata mavuno mengi na yenye tija.

Mmoja wa wanufaika wa mbegu hizo akiongea kwa niaba ya wakulima ndugu Yordan Nguruwe ameshukuru uongozi wa TARI Kwa kuwapatia mbegu bora na yenye tija kwani amesema itasaidia kuongeza kipato kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

# PONGEZI

WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

## PONGEZI



**Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunakupongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

*Tufuatilie* Tari Tanzania | tari.tanzania | TanzaniaTari | TariTV

WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

## PONGEZI



**Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunakupongeza Mhe. Balozi Dkt.Emmanuel Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

*Tufuatilie* Tari Tanzania | tari.tanzania | TanzaniaTari | TariTV

WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

## PONGEZI



**Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunakupongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Muhula wa Pili wa awamu ya Nane.**

*Tufuatilie* Tari Tanzania | tari.tanzania | TanzaniaTari | TariTV



# WAKULIMA WA PAMBA WAHIMIZWA KUACHANA NA KILIMO CHA MAZOEA ILI KUONGEZA TIJA

**WAKULIMA** wa pamba nchini wamehimizwa kutumia teknolojia za kisasa za uzalishaji ikiwepo upandaji wa zao hilo kwa nafasi mpya za upandaji (sm60 x sm30) iliyogunduliwa na TARI ambazo zimekuwa chachu ya kuongezeka kwa uzalishaji wa pamba nchini.

Wito huo umetolewa Novemba 17,2025 na Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt Thomas Bwana katika Mkutano wa wadau wa Mradi wa Cotton Victoria uliofanyika katika kituo cha TARI Ukiriguru (Mwanza) kwa lengo la kutathimini utekelezaji wa mradi. Amesema kutokana na matumizi ya teknolojia zilizoasisiwa na mradi huo, wakulima wameshuhudia mabadiliko makubwa katika uzalishaji.

*"Kuna maeneo wakulima walikuwa wanapata chini ya kilo 500 (kwa ekari) lakini sasa hivi kuna wakulima wanapata zaidi ya kilo 1000, kwahiyo unaweza kuona kwamba ongezeko la mavuno ni kubwa kwa wale wanaotumia mbinu ambazo tumewaelekeza"* amesema Dkt Bwana na kubainisha mbinu hizo ni pamoja na kupanda kwa wakati kwa kutumia umbali wa sm 60 x sm 30, matumizi sahihi ya viuatilifu, na kudhibiti magugu kwa wakati.



Mradi wa Cotton Voctoria ulianza kutekelezwa mwaka 2016 ukiwa na lengo la kuinua uzalishaji wa pamba katika nchi za Tanzania, Kenya na Burudi. Hadi sasa hapa nchini, mapokeo ya teknolojia za mradi huu yamefikia asilimia 63 ya wakulima wa pamba katika Mikoa 11 inayozalisha zao hilo la kibiashara.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania Bw. Marco Mtunga amesema kuwepo kwa mradi huu kumejibu hoja ya kuongeza tija katika uzalishaji wa pamba *"Maeneo kama Simiyu sehemu kubwa ya wakulima walikuwa wana sia mbegu, lakini sasa wanapanda kwa vipimo ambavyo vinatoa idadi kubwa ya miche, na kuchangia uzalishaji kuwa mkubwa kwenye eneo." amesema Bw. Mtunga.*

Mkutano wa kutathimini utekelezaji wa mradi wa Cotton Victoria umewakutanisha wadau mbalimbali katika tasnia ya pamba wakiwemo watafiti kutoka TARI kituo cha Ukiriguru, Bodi ya Pamba, wawakilishi kutoka Wakala wa Ushirikiano wa Brazili (ABC) na ubalozi wa Brazil nchini Tanzania, baadhi ya Maafisa kilimo na wakulima viongozi kutoka Mkoani Geita, pamoja na uwakilishi kutoka Wizara ya Kilimo.









# BILA UTAFITI IMARA HAKUNA TIJA KWENYE KILIMO-DKT. BWANA

**MKURUGENZI** Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa kilimo Tanzania (TAR), Dkt. Thomas Bwana, amesema msingi wa kilimo chenye tija ni utafiti ambao ukiwafikia wakulima na kutekelezwa ipasavyo utatoa matokeo stahiki.

Dkt. Bwana ameyasema hayo katika Mkutano wa Biashara na Uwekezaji wa kilimo cha mbogamboga, matunda, viungo na vikolezo (HcBIS) uliofanyika jijini Dar Es Salaam Novemba 12, 2025 wakati akiwasilisha mada kuhusu mchango wa TARI katika utafiti wa mazao ya "Horticulture".

Amesema TARI inafanya tafiti zinazotatua changamoto za wakulima na watumiaji wa bidhaa hizo ili kuhakikisha tija na ubora unapatikana na kutoa matokeo halisi kwa wakulima na wadau.

Kuhusu mbinu zinazotumika kuwafikia wadau na wakulima, Dkt. Bwana amebainisha kuwa TARI hufanya tafiti shirikishi kwa kutatua changamoto walizonazo wakulima pamoja na kushiriki maonesho mbalimbali ambayo wadau wa kilimo na wakulima huudhuria ambapo elimu ya teknolojia mbalimbali za TARI Pamoja na ushauri hutolewa ili kuhakikisha sekta ya mazao ya mbogamboga, matunda, viungo na vikolezo inakuwa kwa kasi kubwa,

Dkt. Bwana ametowa wito kwa wadau hususuani wakulima kuzingatia matokeo na matumizi ya tafiti ili kutekeleza kilimo cha kisasa chenye tija.

Katika hatua nyingine, Mtafiti kutoka Kituo cha TARI Tengeru Dkt. Happyness Molel amewaomba watafiti kutoka Taasisi hiyo hasa Vituo vinavyofanya tafiti za mbogamboga, matunda, viungo na vikolezo kuendeleza tafiti za mazao hayo ili kuwasaidia wakulima na kuwawezesha kutambua changamoto na fursa zilizopo katika sekta ya mazao hayo ndani na nje ya nchi ili kupata matokeo chanya.

Mkutano huo ulioandaliwa na TAHA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo watafiti wa TARI kutoka Vituo vya TARI Tengeru, TARI Makutupora, TARI Mlingano, TARI Maruku, TARI Uyole, TARI Tumbi, TARI Dakawa, TARI Kifyulilo, TARI Naliendele na TARI makao makuu.

Aidha, kupitia Mkutano huo TARI ilipata fursa ya kuonesha bidhaa mbalimbali za mbogamboga, matunda viungo na vikolezo pamoja na kujadiliana na TAHA kuona namna Taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana na kufanyakazi pamoja ili kuhakikisha sekta ya mazao hayo ya mbogamboga, matunda, viungo na vikolezo inaboreshwa zaidi.





*Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu Dkt. Deusdedith Mbazibwa (kati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watafiti wa Kituo cha TARI Kihinga.*

# MKURUGENZI WA UTAFITI NA UBUNIFU AKAGUA MIRADI YA UTAFITI KATIKA KITUO CHA TARI KIHINGA

**MKURUGENZI** wa Utafiti na Ubunifu (DRI) wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt. Deusdedith Mbanzibwa alitembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo kilichopo TARI-Kihinga tarehe 21 Desemba 2025 kwa lengo la kufuatilia na kukagua maendeleo ya miradi na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa kwa mujibu wa majukumu ya kituo hicho.

Katika ziara hiyo Dkt. Mbazimbwa alipata fursa ya kutembelea mashamba mbalimbali ya majaribio ya utafiti na pia alipata maelezo ya kina kuhusu shughuli za kila siku zinazoendeshwa na kituo hicho mahsusi kwa zao la chikichi katika kanda ya Magharibi mwa Tanzania.

Dkt. Mbazibwa aliuagiza uongozi wa kituo hicho kuboresha mwongozo wa kilimo bora cha zao la chikichi ili kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kwa kilimo endelevu chenye tija.

Aidha, alipata nafasi ya kujadiliana na watumishi wote juu masuala yanayohusu utafiti na ubunifu, changamoto zinazowakabili watafiti na fursa za kuboresha utendaji kazi kwa matokeo yenye ufanisi.

Hata hivyo, Dkt. Mbazibwa alisisitiza watafiti kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kutumia rasilimali fedha na rasilimali nyinginezo kwa umakini ili kuhakikisha thamani ya pesa inaakisi maendeleo endelevu ya kituo na kufikia malengo ya taasisi yaliyokusudiwa.



*Mtafiti, Madili Kuzenza kutoka TARI Kihinga akitoa maelezo kwa Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu Dkt. Deusdedith Mbazibwa kuhusu uzalishaji wa miche ya chikichi.*

# VITUO VYA UTAFITI VYAFANYA MKUTANO WA MAPITIO YA SHUGHULI ZA UTAFITI WA KILIMO NA UHALISHAJI WA TEKNOLOJIA



*Mgeni Rasmi Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa Bi. Elina Dastan Akizungumza katika mkutano wa mapitio ya shughuli za utafiti vituo vya TARI Dakawa, TARI Ilonga na TARI Ifakara.*

**VITUO** vya TARI Ilonga, TARI Dakawa na TARI Ifakara, vimefanya mkutano wa mapitio ya ndani ya shughuli za utafiti wa kilimo na uhaulishaji wa teknolojia (Internal Pragramme Review - IPR) kuanzia tarehe 16 hadi 17 Desemba, 2025 katika ukumbi wa MATI Ilonga.

Mapitio hayo ni sehemu ya mkakati wa TARI wa kuhakikisha utafiti na uhalishaji wa teknolojia unafanyika kwa weledi kwa kuzingatia misingi ya kisayansi na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Akizungumza katika mkutano huo, Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huo Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa Bi. Elina Dastan amesema kuwa mapitio hayo yanawawezesha wadau wa kilimo kushirikiana kutathmini changamoto na mafanikio katika utafiti wa kilimo, hatua itakayosaidia kuimarisha kilimo chenye tija na endelevu katika Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, kiongozi wa timu ya mapitio Dkt. Nessie Luambano alibainisha kuwa mapitio hayo yanasaidia kubaini changamoto za utekelezaji na kuweka mikakati ya kuzitatua, huku akisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wanasayansi wachanga ili kuwajengea uwezo na ujuzi wa kitafiti.

Mapitio hayo ya ndani ya shughuli za utafiti yameviwezesha vituo vya TARI kutathmini kwa kina utekelezaji wa programu zake za utafiti na uhaulishaji wa teknolojia ili kubaini maeneo ya kuboresha na kujiimarisha zaidi katika kuzalisha teknolojia na bunifu zitakazochochea maendeleo ya kilimo endelevu nchini.

Mikutano ya mapitio ya ndani ya shughuli za utafiti yaani -(IPR) kwa mwaka 2025 imefanyika katika kanda zote saba:

Kanda ya Kaskazini inayohusisha vituo vya TARI Selian na TARI Tengeru; Kanda ya Mashariki (1) inayohusisha vituo vya TARI Mlingano, TARI Kibaha na TARI Mikocheni; Kanda ya Kati ikihusisha TARI Makutupora na TARI Hombolo; Kanda ya Mashariki (2) ikihusisha vituo vya TARI Dakawa, TARI Ifakara na TARI Ilonga; Kanda ya Magharibi inayohusisha vituo vya TARI-Tumbi na TARI-Kihinga;

Kanda ya Kusini inayohusisha kituo cha TARI-Naliendele; Kanda ya Ziwa ikihusisha vituo vya TARI Maruku na TARI Ukiriguru pamoja na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayohusisha vituo vya TARI Uyole na TARI Kifyulilo. Mikutano hii ya "IPR" inasaidia kuleta wadau wa utafiti pamoja, kupitisha maandiko miradi ambayo hupelekwa kwa wafadhili.



VIUNGO NA VIKOLEZO

# JE, WAJUA?



**MTI** wa "Allspice" (Pimenta dioica) ni mti wa Kiafrika unaotoa viungo vinavyochanganya ladha za mdalasini, karafuu, na tangawili (nutmeg), ukitumika sana kwenye vyakula, dawa, na chai?.

**Jina:** "Allspices", au Pimento, na kwa Kiswahili unajulikana kama "Mti wenye mchanganyiko wa viungo vyote" (TARI).

Kwa mujibu wa Mtafiti Dkt. Mgaya Maumba kutoka Kituo cha TARI Mlingano Tanga wanaojihusisha na utafiti wa Viungo na vikolezo, mti huu unaitwa *allspice* au mchanganyiko wa viungo vyote, ni mti mmoja ambao umekusanya kiungo zaidi ya kimoja katika harufu yake, ukinusa majani yake utahisi harufu ya viuongo mbalimbali kama karafuu, iliki na mdalasini.

Majani ya mti huu hutumika kama kiungo katika mapishi ya vyakula mbalimbali kama na vinywaji kama chai, supu, biriani, pilau na hata katika *ice cream* au sehemu ya kuokea mikate. Kiungo hiki kina manufaa makubwa kiafya kwani




husaidia mmeng'enyo wa chakula.

Wataalamu wanashauri watu watumie zaidi majani kwa kuwa wakitumia magome wataua mti.

Miche ya kiungo hiki cha *allspices* inazalishwa na Kituo cha TARI Mlingano. Kwa mahitaji ya miche ya kiungo hiki na viungo vingine pamoja na vikolezo wasiliana na Kituo chochote cha TARI kilicho karibu yako.

# PONGEZI


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba
Kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa
Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
PONGEZI
Mhe.Mussa Azzan Zungu
Kwa kuchaguliwa kuwa spika wa
Bunge la Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania 2025-2030
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV






# TARI NA JIRCAS KUSHIRIKIANA KATIKA UTAFITI WA KILIMO

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imepokea ujumbe kutoka Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Kilimo cha Japan (JIRCAS) kufuatia ziara iliyofanyika leo, tarehe 11 Desemba 2025. Ujumbe huo uliongozwa na Dkt. Hirouchi Shinji, akifuatana na Dkt. Onishi Junya pamoja na Bw. Yona Anderson kutoka Chuo cha Ufundi Arusha.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kiongozi wa msafara, Dkt. Shinji, alieleza kuwa lengo la ziara hiyo ni kuimarisha ushirikiano na Tanzania katika maeneo makuu sita (6) ya kipaumbele, yakiwemo uzalishaji wa chakula, maendeleo ya wakulima na Sekta Binafsi, uboreshaji wa Lishe, hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, Dkt. Shinji alibainisha kuwa JIRCAS imekusudia kushirikiana na TARI kuboresha na kuendeleza aina za mpunga zinazostahimili ukame, ikiwa ni sehemu ya mpango mkakati wa kuunga mkono mifumo endelevu ya uzalishaji wa chakula nchini kwa kuwa Taasisi yake inajishughulisha na kusaidia nchi zinazoendelea.

Kwa upande wa TARI, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. George Sonda alisema kuwa Taasisi inajukumu la kufanya utafiti na kusambaza matokeo kwa wadau wa kilimo pamoja na kutoa ushauri kwa watunga sera.

Aidha, alisema kuwa ushirikiano huu mpya utakuwa na mchango mkubwa katika maeneo yanayolima mpunga, hususani katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji.

Mbali na TARI, JIRCAS pia inashirikiana na taasisi nyingine za ndani ikiwemo Chuo cha Ufundi Arusha na NiRCI. Inatarajiwa kuwa mara baada ya kuwasilishwa kwa miradi husika, makubaliano ya utekelezaji yatafikiwa baina ya JIRCAS na taasisi zote inazoshirikiana nazo nchini.





# KIJUE KITUO CHA TARI KIHINGA

**TARI** Kihinga ni moja kati ya Vituo 20 vya TARI kilichoanzishwa mwaka 2018 kwa lengo la kufanya na kuratibu utafiti wa kina kuhusu zao la michikichi. Kuanzishwa kwa kituo hiki ni hatua kubwa katika kuimarisha uwezo wa Tanzania kuongeza uzalishaji na tija ya zao la michikichi kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi, kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje na kukuza uchumi wa taifa na wa mtu mmoja mmoja.

Kituo hiki ambacho kiko Kata ya Mungonya Mkoani Kigoma ni kitovu cha Kitaifa cha utafiti wa zao la michikichi, kikijikita zaidi katika maeneo yote muhimu ya mnyororo wa thamani wa zao hili, yakiwemo:

- Uboreshaji wa miche na mbegu
- Teknolojia za kilimo (agronomia)
- Udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu
- Usimamizi wa mavuno na baada ya mavuno
- Uzalishaji wa mbegu na miche bora
- Kutoa ushauri kuhusiana na kanuni za kilimo bora cha chikichi.




TARI Kihinga imejidhatiti katika kubuni na kusambaza aina bora na zilizoboreshwa za michikichi zinazokidhi mahitaji ya wakulima na zinazolingana na ajenda ya mageuzi ya kilimo nchini. Kupitia shughuli hizi, Kituo huhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kupanda vinavyosaidia:

- Kuongeza mavuno
- Kuongeza ustahimilivu dhidi ya magonjwa na wadudu
- Kuboresha ubora wa mafuta ya mawese

Mbali na michikichi, TARI Kihinga hushirikiana na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi katika kufanya utafiti wa mazao mengine muhimu kama vile mihogo, maharage, ndizi, mahindi na parachichi. Utafiti huu mseto huimarisha wigo wa Kituo katika kutoa suluhisho la kilimo shirikishi, na kuchangia katika usalama wa chakula na kuongeza kipato cha wakulima nchini.

# TARI SEED 105

## SIFA ZAKE

- Yana stawi vizuri katika ukanda wa chini na wa kati mita 0-1500m kutoka usawa wa Bahari
- Hustahimili ukame
- Hukomaa mapema (wastani wa siku 110-125)
- Hutoa mavuno mengi, wastani wa gunia 20-22 kwa ekari
- Yanakoboleka vizuri
- Yanapunje nene
- Matamu kwa kuchoma, hivyo yanafaa kwa kilimo cha bustani.
- Aina ya mbegu ina ukinzani na magonjwa mbalimbali kama: milia ya mahindi (MSV), Bakajani kijivu (Gray leaf sport) na kutu ya majani (Leaf rust).

## UPANDAJI

Mbegu moja kwa shimo: sm 75 x 25-30

Mbegu mbili kwa shimo  sm 75 x 50-60



# PONGEZI


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
PONGEZI
Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa
Taasisi ya Utafiti wa KilimoTanzania (TARI) tunakupongeza
Mheshimiwa Daniel Chongolo
kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
kuwa Waziri wa Wizara ya Kilimo.
Utafiti kwa Maendeleo ya kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
PONGEZI
Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa
Taasisi ya Utafiti wa KilimoTanzania (TARI) tunakupongeza
Mheshimiwa David Silinde
kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo.
Utafiti kwa Maendeleo ya kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


TariTanzania
TUFUATILIE MITANDAONI
Tanzaniatari
TariTV
official_taritanzania

# HABARI KATIKA PICHA



MHE.DANIEL CHONGOLO, WAZIRI WA KILIMO AKIPOKEA MAELEZO YA TEKNOLOJIA YA KITALU NYUMBA KUTOKA KWA MKURUGENZI WA KITUO CHA TARI NALIENDELE DKT. GERADINA MZENA.



WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI WA TARI NA MENEJIMENTI YA TARI KATIKA PICHA YA PAMOJA MARA BAADA YA KIKAO CHA BODI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA ST.GASPER MKOANI DODOMA.



MENEJIMENTI YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA(TARI) MAKAO MAKUU, TARI MAKUTOPORA PAMOJA NA MAAFISA KUTOKA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA WAKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA.



MTAFITI KUTOKA TARI BWANA WATSON GWIDO MATAMWA AKIWAPATIA ELIMU YA NAMNA BORA YA UTUNZAJI WA UDONGO WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI DODOMA KWA UPANDAJI WA MTI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA UDONGO DUNIANI.



MSIMAMIZI WA KITUO CHA UHAULISHAJI TEKNOLOJIA CHA NGONGO MANISPAA YA LINDI BI.BAKINA OBADIA MSALILWA AKIONESHA BAADHI YA MAZAO YA MBOGAMBOGA NA MATUNDA YANAYOLIMWA KATIKA KITUO HICHO.



MHE.DANIEL CHONGOLO, WAZIRI WA KILIMO AKIPOKEA ZAWADI KUTOKA KWA MKURUGENZI WA KITUO CHA TARI NALIENDELE DKT.GERADINA MZENA



WATUMISHI WA TARI WAKISHIRIKI MCHEZO WA KUKIMBIA NA MAGUNIA.

# WATUMISHI WAHIMIZWA KUSHIRIKI MICHEZO KUBORESHA MAHUSIANO MAHALA PA KAZI

**WATUMISHI** wa Taasisi ya kilimo Tanzania (TARI) wameaswa kudumisha utamaduni wa kufanya michezo ili kuboresha afya pamoja na kudumisha mahusiano mahali pa kazi.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimali watu na Utawala wa TARI, Zephania Mshanga katika bonanza la michezo lililofanyika Oktoba 25, 2025 katika viwanja vya shule ya sekondari Dodoma.

Bonanza hilo liliandaliwa na vituo vya TARI Makutupora na TARI Hombolo ambapo watumishi wa TARI Makao Makuu pia wameshiriki Bonanza hilo ambalo lilipambwa na michezo mbalimbali ikiwepo kukimbia, kuvuta Kamba, mbio za magunia, kupuliza puto, kukimbiza kuku, mpira wa miguu pamoja na mazoezi ya viungo ambapo washindi mbalimbali wamepata Zawadi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mkurugenzi wa kituo cha TARI Makutopora Dkt Amarchius James na Meneja wa kituo cha TARI Hombolo Dkt. Emmanuel Chilagane walipongeza watumishi kwa kushiriki bonanza hilo huku wakisisitiza umuhimu wa kufanya michezo ili kuboresha afya zao pamoja na kujenga mahusiano baina ya watumishi.

Mbali na bonanza hilo, TARI imejenga utamaduni wa kushiriki masuala ya michezo ambapo TARI kituo cha TARI Naliendele kimeshiriki mbio za Korosho Marathon ambazo zimekuwa zikifanyika kila mwaka mkoani Mtwara.

Pamoja na umuhimu wa michezo kituo hicho kimetumia michezo kama fursa ya kutoa elimu ya kilimo bora, uongezaji thamani wa zao la Korosho na ugawaji wa mbegu bora za korosho kwa wakulima.

Pia, katika kutambua mchango unaotolewa na wadau katika maendeleo ya Kilimo Tanzania, TARI Uyole imeshiriki ligi ya Prof. Mbwette Memorial Cup ambayo inashirikisha Vijiji Saba vya Kata mbili za Mbeya Vijijini ambazo ni Ulenje na Maendeleo.

Kwakutambua ukubwa wa tukio hilo TARI kwa kushirikiana na wadau wengine sambamba na burudani hiyo imehakikisha wakulima wanapatiwa elimu kuhusu kilimo bora kwa njia ya mashamba darasa ambapo TARI Uyole imesambaza teknolojia mbalimbali za mazao ya mahindi, ngano, ulezi, alizeti, viazi mviringo na pareto.



WATUMISHI WA TARI WAKISHIRIKI BONANZA LA MICHEZO (MCHEZO WA KUVUTA KAMBA)



WATUMISHI WA TARI WAKISHIRIKI MCHEZO WA KUPULIZA MAPUTO



WATUMISHI WA TARI WAKISHIRIKI MCHEZO WA KUKIMBIA NA MAYAI KWENYE KIJIKO.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

# VITUO VYA UTAFITI TARI





**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)**
**S. L. P 1571, Dodoma**
**Tel: +255 26 2961 993/e-mail:dg@tari.go.tz**
**Website:www.tari.go.tz**


TariTanzania  tari.tanzania  Tanzaniatari  TariTV